JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA
SHULE YA SEKONDARI RUANGWA

S.L.P 47,
RUANGWA,
01/05/2022.

SIMU: Mkuu wa shule – **0769 -323 079 / 0710 401 999**

Email *ruangwasecondaryschool@gmail.com*

Makamu mkuu wa shule – **0786 240 629/0753 100 951**

KUMB.NA.RSS/R.2/VOL.2/2022.

JINA LA MWANAFUNZI ……..

S.L.P ……...

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO 2022

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Nachukuwa nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri katika mtihani wako wa kidato cha nne mwaka 2021. Ninayofuraha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari **RUANGWA** katika mchepuo (Combination) wa ……

Shule ya sekondari Ruangwa ipo umbali wa Kilomita 1.5 mashariki ya Mji wa **RUANGWA** ambao ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Ruangwa Mkoani Lindi. Utakapofika Ruangwa mjini chukua usafiri wa pikipiki au Bajaji au Tax utalipa kati ya 1000/= usafiri wa pikipiki na 3000/= usafiri wa bajaji/tax hadi kufika shuleni. Kwa wanaotokea au kupitia Dar es Salaam, mabasi ya Ruangwa, yanapatikana kituo cha mabasi cha Sudani au Temeke mwisho au kituo cha mabasi Mbagala.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ambazo unatakiwa kuzisoma kwa makini na kuzifanyia kazi.

i. Fomu ya mahitaji muhimu ya shule
ii. Fomu ya kupimwa afya ya Mwanafunzi kutoka kwenye Hospitali inayotambulika na Serikali.
iii. Fomu ya taarifa za Mwanafunzi na Mzazi/ Mlezi.
iv. Fomu ya sheria za shule
v. Mkataba wa Mwanafunzi wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.

Shule itafunguliwa tarehe **……..** Nafasi yako itatunzwa kwa muda wa siku 14 kuanzia tarehe ya ufunguzi wa shule. Hivyo kamilisha mahitaji mapema na kuwahi shule kabla nafasi yako haijajazwa na mtu mwingine endapo utachelewa.

NB: Unatakiwa kuja na **Result Slip, nakala ya Cheti cha kuzaliwa na picha (passport size 2)**.

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja Ruangwa Sekondari.

KARIBU SANA!
"JUHUDI NA NIDHAMU HULETA MAFANIKIO"

…….
GILBERT M. ASSEY
MKUU WA SHULE.

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

1.0 Sare za Shule.

i. Suruali mbili (2) za Light Blue zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo.
ii. Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu na yenye kola shingoni.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi (2) viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vya kupanda
iv. Tai ya rangi ya light blue
v. Soksi imara nyeusi jozi mbili (2)
vi. Nguo za michezo, bukta moja, T-shirt ya blue, Track suit ya blue na viatu vya michezo.
vii. Aje na sweta moja (1) rangi ya Blue liwe la kufuma.
viii. Suruali nyeusi mbili (2) (shamba dress) na T-shirt mbili (2) za blue isiyo na maandishi.

NB: Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare zilizoanishwa hapo juu muda wote, na hata awapo safarini na haruhusiwi kuja na nguo yoyote ya nyumbani.

MSISITIZO

Wazazi/Walezi na wanafunzi wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kuhusu sare na uvaaji wa sare. Wakati mwingine wanafunzi kwa matakwa yao binafsi huamua kushona suruali iliyobana na iliyochongolewa. Mavazi ya aina hiyo hayatakubaliwa. **EPUKA USUMBUFU NA KERO MAPEMA. ZINGATIA MAELEKEZO ULIYOPEWA.UTAKAPORUDISHWA KWA SABABU YA KUTOZINGATIA MAAGIZO YALIYOTOLEWA USIJE KULALAMIKA WALA KUMLAUMU MTU YEYOTE.**

1.1 Mahitaji kwa ajili ya malazi

i. Godoro la sponji moja 2½, x 6''
ii. Shuka mbili (2) za rangi ya bluu bahari iliyoiva
iii. Chandarua rangi ya blue chenye dawa kwa ajili ya kujikinga na Mbu wanaoambukiza malaria.
iv. Mto na foronya yake.
v. Taulo moja.
vi. Sanduku la chuma (bati) linalofungwa na kufuli.

1.2. Mahitaji kwa ajili ya chakula

(a) Sahani (b) Bakuli (c) Kikombe (d) Kijiko

1.3 MAHITAJI KWA AJILI YA TAALUMA

(a) Ream mbili (2) za karatasi za photocopy (A4) zitakazokabidhiwa siku ya kuripoti shuleni (b) Daftari za kutosha kulingana na masomo yako (c) kalamu ya wino wa blue au mweusi na kalamu ya risasi au penseli (d) vitabu vya masomo kulingana na tahasusi aliyochaguliwa (HGK, HKL na HGL (e) mafaili mawili (plastic folder).

1.4 VIFAA VYA USAFI

(a) Fyekeo (b)Panga (c) Jembe (d) Fagio (e) Sqeeser /Mopper (1) (f) Ndoo ndogo mbili (g) Fagio ngumu la chooni (1), (h) Reki(1)

N.B Vifaa hivi vinapatikana shuleni, hivyo mzazi / mlezi kuondoa usumbufu wa usafirishaji utavipata kwa bei nafuu hapa shuleni.

2. KARO NA MICHANGO YA SHULE

(a) Karo ya shule ni **Tshs. 70,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa yote kwa wakati mmoja au Tshs. 35,000/= kwa muhula, kila mwanzo wa muhula.

(b) **Michango mingine inayotakiwa kulipwa Shuleni**

i. Kitambulisho na picha Tshs 6,000/=
ii. Tahadhari Tshs 5,000/=[Haitarejeshwa]
iii. Mchango wa ukarabati wa samani Tshs 15,000/=
iv. Taaluma kwa mwaka Tshs 20,000/=
v. Mchango wa walinzi,wapishi na vibarua kwa mwaka Tshs 35,000/=
vi. Nembo ya shule sh. Tshs 2,000/=
vii. Mchango wa huduma ya afya shuleni 10,000/= (Huduma ya kwanza Tshs 5000/= Bima ya Afya 5000/=)
viii. Mtihani wa pamoja (UTAMIRIFU) KIDATO cha Tano Tshs 20,000/=
ix. . Mchango wa Umisseta 5,000/= kwa mwaka.

NB: Michango yote ilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. 71101100094 NMB (RUANGWA Secondary School Recurrent Account). Tafadhali wasiliana na karani wa Benki aandike kuwa ni ada au michango mingine. Usisahau kuandika jina lako kamili (Mwanafunzi). Risiti (paying slip) utakuja nayo siku ya kufungua shule. Mwanafunzi hatapokelewa endapo hajakamilisha michango husika.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESDENT'S OFFICE; REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

RUANGWA DISTRICT COUCIL

RUANGWA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 47,

RUANGWA.

01/05/2022

REF. No……

THE MEDICAL OFFICER……

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ……

Please Examine the above-named pupil and give us a regarding his/her suitability for Secondary School studies.

1. Pupil's full name ……..…….
2. Blood.....
3. Stool.....
4. T.B test.....
5. Syphilis test.....
6. Urine examination ……....
7. Eye test.....
8. Chest.....
9. Ear.....
10. Spleen.....
11. Abdomen test.....
12. Pregnant test (girls only) ……..……..……..

I certify that the above pupil is suitable/for studies

If unsuitable please give reasons **.....**

……

Name of MEDICAL Officer.....

Signature of Medical Officer ……

Date.....

Official Stamp.....

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

SHULE YA SEKONDARI RUANGWA

FOMU YA KUJIANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA MZAZI NA MWANAFUNZI.

SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi) ……
2. Tarehe ya kuzaliwa …….

3. Kabila ……..

4. Mahali na Wilaya alipozaliwa …….

5. Shule alipomaliza Darasa la Saba …….. ……

6. Kidato anachokuja kuingia …….

7. Michezo anayopendeleya

1	
2	
3	

UONGOZI WA SHULE

Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile. Kiranja, Kiongozi wa Kwaya, Ngoma Michezo n.k.

S/N	NAFASI YA UONGOZI	SHULE	MWAKA
1			
2			
3			

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kamili na za ukweli

Tarehe …… **saini……**

SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

i. Jina kamili.....

ii. Kazi.....

iii. Nyumbani.....

iv. Kata.....

v. Tarafa.....

vi. Anwani ya Mzazi/Mlezi …….

vii. Namba ya simu …….

viii. Dini ……

ix. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo……

Ninaahidi kushirikiana na Walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya kusoma.

Mimi ……. Mzazi/Mlezi ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi

Tarehe …… saini……

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha unatakiwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa Walimu, Viongozi, Wazazi na Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika shule hii.

e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

f) Kuvaa sare ya shule kwa unadhifu wakati wote unapotakiwa.

g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

h) Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele.

i) Shule haimfungi Mwanafunzi kuamini katika imani yake ila kwa muda maalum na siku maalum .

j) Hatakiwi kuja na nguo za nyumbani.

k) Mwanafunzi Ajapo kuripoti, aje na Mzazi. **Bila kuja na Mzazi hatapokelewa**

l) Ni marufuku kuendesha ibada wakati wa masomo au kikao chochote bila kibali maalumu

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.

1. **Wizi**

2. Uasherati na Ushoga

3. Ubakaji.

4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.

5. Kupigana au kupiga

6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.

7. Kudharau Bendera ya Taifa

8. Kuoa

9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule

10. Kusababisha mimba ndani au nje ya shule.

11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

12. Kukataa adhabu.

13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

14. kuzurura mitaani / mjini au kwenye mapori wakati wa shule bila ruhusa maalumu.

15. **MWANAFUNZI ATAKAYE KUTWA ANACHAFUA KUTA ZA SHULE ATALAZIMIKA KULIPA NDOO (1) YA RANGI PAMOJA NA TSHS 10,000/= ZA UFUNDI IKIWA NI PAMOJA NA KUFUKUZWA SHULE.**

Muhimu

Mwanafunzi atatakiwa kufuata kanuni zote zitakazo elekezwa au atakazo zikuta mara atakapo jiunga na shule hii.

Mwanafunzi atalazimika kutumia utashi wake wote kupambanua kila jambo kwani kutokujua kosa hakutazuia yeye kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na taratibu za shule

MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ……..nimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule. Kwa hiari yangu nakubaliana nayo.

Naahidi nitaheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha naahidi kuwa kwavyovyote vile sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sheria, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo, fujo na kutenda makosa ya jinai, basi nichukuliwe hatua ya stahiki kulingana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya Mwanafunzi .....

Saini ya Mzazi.....

Saini ya Mkuu wa shule ……